


# Pambazuko Ukweli Hauna Kutu

Toleo Namba 00002

Jumatatu-Julai 18, 2022

GHARAMA ZA MAISHA...



## Nani hasa anafaidi maisha magumu?

- *Kaya zianze kuondoa umasikini wa kudumu*

### YALIYOMO

Uk-4: Haya ya-jengewe mnara

Uk-5: Samia atamani kuwa Samia

Uk - 7: Mhubiri bangi kura rais?



**JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure**

## Anza, dumu na Pambazuko

**L**eo, Jumatatu ya Julai 11, 2022 - wewe unakuwa mmoja wa wasomaji wa kwanza wa gazeti la Pambazuko, ambalo litakuwa likikufikia bila gharama yoyote kupitia njia za kisasa za mawasiliano; simu yako ya mkononi na hata kompyuta.

Pambazuko ni gazeti-teke linalochapishwa kwa Kiswahili na kusambazwa kwa njia rahisi ya WhatsApp na mifumo mingine ya mitandao ya kijamii, kwa lengo kubwa la kusambaza habari zilizofanyiwa kazi kwa kuzingatia miiko yote ya kukusanya na kuchakata habari kabla ya kufikia umma; ikiwa ni pamoja na habari za kweli, zenye kuzingatia staha ya binadamu na utu wake.

Ni gazeti lililosajiliwa na Serikali ya Tanzania na kuanza kuhaririwa katika nchi hiyo, lakini kila baada ya muda maalum, litakuwa likihamisha usimamizi kwenda nchi nyingine ambako kuna wahariri wake; Kenya, Uganda na Rwanda,

Gazeti hili, pamoja na kusambaza habari, pia ni uwanja mpana wenye fursa kwa kila mmoja kutoa maoni yake na kuhakikisha kupitia Pambazuko, yanafika kwa taasisi zenye kisimamia nguzo za uamuzi katika nchi; serikali, bunge na mahakama.

Pamoja na kuwa gazeti hili ni chombo cha dunia, kwa imani kwamba kupasha habari hakuna mipaka kwa sasa, lakini walengwa wakubwa wa awali ni watumiaji wa lugha adhimu ya Kiswahili- ikiwa ni pamoja na

wanafunzi wa lugha hiyo - wengi wakitoka Afrika na wengine wakiwa maeneo mengine nje ya bara hilo.

Katika kuhakikisha Kiswahili kinakua na 'kupasua anga,' kurasa moja ya Pambazuko, itabeba darasa la kufunza kwa yeyote anayependa kuelewa lugha hiyo inayokadiriwa kuwa na wazungumzaji wanaozidi milioni 300 duniani.

Msukumo wa kuanza Pambazuko umejengeka katika misingi mingi, mkubwa ukiwa ni kukubalika kwa wazo letu kwa wadau na kushikwa mkono na marafiki wa haki ya kupata habari, Simon Allison, Kiri Rupiah na timu ya gazeti la The Continent. Tunashukuru sana.


Ombi letu kubwa kwako msomaji wa Pambazuko, ni kusaidia kusambaza gazeti hili kwa marafiki wote, ndugu na jamaa ili kila mmoja apate haki hii na kuwa chanzo cha kukuza maarifa na kutambua kinachoendelea duniani.

Tunaomba kila mmoja awe balozi wa kazi hii iliyotukuka ambayo, pamoja na gharama zake, tumeamua kuibeba na kuifanya bure kwa sasa.

Sisi binadamu, tusifurahie Ukuu wa Mungu pekee kwa kupambazua siku, bali kwa kuanza kusoma Pambazuko kila Jumatatu ili kupata fursa zaidi ya habari.

Karibu sana.

Simon Martha Mkina



## Jisajili kupata Pambazuko bure

Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya WhatsApp: +255 744 768263 na kutuma neno “HABARI” ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

Pia unaweza kujisajili kwa kutumia Email hii: [pambazuko1@protonmail.com](mailto:pambazuko1@protonmail.com) ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno “HABARI” na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

### Tuwe wavya kupata Katiba mpya



Rais Samia Suluhu Hassan

#### Na Plato Hekimachus

**H**IVI karibuni Chama Cha Mapinduzi (CCM) kilifanya uamuzi wa kihistoria kwa kuridhia kufufua mchakato wa kupatikana kwa Katiba mpya nchini Tanzania.

Uamuzi huo ulikuwa umezima - kwa muda, kelele za madai ya katiba mpya ambazo zimekuwa zikipazwa na Watanzania wengi, hata kama CCM wenyewe wanadai vinginevyo.

Pamoja na uamuzi huo kuonyesha utayari, zipo hisia kwamba huenda umefanywa kwa nia iliyojificha kuliko dhati inayoonekana ama kusikika kutoka kwa baadhi ya viongozi wa chama hicho tawala.

Mchakato wa kupatikana kwa Katiba mpya ulianzishwa na kumalizwa na Rais Jakaya Kikwete mwenyewe, ambaye awali aliuaminisha umma kwamba kabla ya kuondoka kwake madarakani, Novemba 5, 2015, angeacha Tanzania ikiwa na Katiba mpya ambayo huenda ingekuwa na majawabu ya changamoto

nyingi zinazozinga ustawi wenye neema kwa wananchi wake.

Kimsingi, uamuzi huo umeibua “tuhuma nzito dhidi ya CCM.” Kwamba watu wanahoji ikiwa kweli CCM imeamua kwa dhati au imewapa watanzania “mdoli” ili wachezee na kupunguza kelele? Tuhuma hizi zisipuuze kwa sababu zina mashiko.

Mmoja wa kada maarufu na mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM amesikika akisema, “tumeridhia mchakato uanze, lakini hatukusema ni lini? Yaweza kuwa baada 2025”.

Mmoja wa makamu mwenyekiti mstaafu amesema -“tumeruhusu, lakini hatukusema tuanzie wapi?”

Kauli hizi mbili zinaashiria hitaji la mjadala mpana wa ujio wa katiba mpya hapa nchini.

Kinachoonekana wazi ni hitaji la watu wavya wa kutuletea katiba mpya. Tunahitaji viongozi wavya na wananchi wavya ili katiba mpya iwezekane kupatikana.

Watu wa zamani hawawezi kutuletea katiba mpya. Baadhi ya watu wa zamani ni wale ‘waliotekwa’ na kuvuruga mchakato ule wa awali. Waliotekwa na waliotekwa katika mchakato ule wanahitaji kufanywa wavya ili waweze kutuletea Katiba mpya.

Maswali ya msingi yanayohitaji ujya wa wahusika ni tuanze lini? Tuanzie wapi? Tukamilishe lini na kwa nini?

Majibu ya maswali haya yamepatikana kutoka kwa Watanzania ambao wanaamini kuna manufaa makubwa kuwa na Katiba mpya kuliko kuendelea kuweka viraka kwenye Katiba ya zamani ambayo imejaa mazingira ya chama kimoja na uimla unaopitwa kwa kasi na mazingira ya sasa.

Ni vyema basi, Katiba mpya ikapatikana mapema kuliko kusubiri wakati mwingine ambao unaweza kuleta ukakasi na kuonekana hata walioshabikia uamuzi wa CCM, waliamua “kuwapaka wananchi mafuta kwa mgongo wa chupa” kwa maslahi ya chama chao na binafsi.

**Gambia**

**Mkuu wa Ujasusi kunyongwa**

**M**KUU wa Idara ya Ujasusi ya Gambia, Yankuba Badije, amehukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa kosa la kumuua mpinzani wa serikali mwaka 2016.

Hukumu hiyo imetolewa wiki iliyopita na Mahakama Kuu ya Gambia baada ya Badije na wasaidizi wake watano wa idara hiyo ,kukutwa na hatia ya kumuua mwanasiasa na mwanaharakati, Ebrima Solo Sandeng.

Badije ambaye sasa ni mstaafu, alitekeleza mauaji hayo kwa kutumia nafasi yake na kwamba alifanya hivyo ili kufurahisha kiongozi aliyemtea kwa nafasi hiyo, Rais Yahya Jammeh.

**Umeme**

**Bilioni 54/- kuwasha umeme visiwani**

**S**ERIKALI ya Tanzania imetenga Sh. bilioni 54 kwa ajili ya kusambaza umeme kwa visiwa zaidi ya 47 ambavyo havijawahi kuona mwanga wa nishati tangu kupata uhuru kwa nchi hiyo Desemba 9, 1961 – miaka 61 iliyopita.

Kiasi hiki ni kikubwa kuwahi kutolewa na serikali kwa ajili ya wananchi wake wanaoishi na kuendesha maisha yao huko visiwani na kwamba hatua hii itasaidia kupunguza umasikini kwani itachochea shughuli za “kutengeneza fedha.”

Waziri wa Nishati, Januari Makamba amesema kwamba fedha hizo zitatumika kwa mwaka huu wa fedha 2022/2023 na kuahidi kusimamia kwa karibu utekelezaji wa bajeti hii ili jambo hili likamilike.



**Nigeria**

**Tiwa atunukiwa udaktari**

**M**WANAMUZIKI wa Nigeria, Tiwa Savage ametunukiwa shahada ya udaktari kutoka Chuo Kikuu cha Uingereza kiitwacho Kent, kwa kutambua mchango wake katika jamii, hasa kuhamasisha vijana kujituma kufanya kazi ili kufanikiwa maishani.

Tiwa, ambaye jina lake la kuzaliwa ni Tiwatope (alibadili) alipewa shahada ya juu ya heshima baada ya baraza la chuo hicho kuridhika kwa mchango wake kwa jamii kupitia muziki. Tiwa ni maarufu duniani kwa kutunga na kuimba mashairi yenye mafunzo na siyo “kubwabwaja.”

Akiwa na mamilioni ya ‘followers’ kwenye mitandao ya kijamii, mwanamuziki huyo aliyemba wimbo maarufu wa Its All Over na Someone’s Son akimshirikisha mwanamuziki wa Marekani, Brandy.

## Hapa na Pale

6

### Nigeria

## Wafugaji konokono waiangukia serikali

**W**AFUGAJI wa konokono wameilalimikia serikali ya Nigeria kwamba imeshindwa kuwathamini na kuwasaidia licha ya kuwa na mchango mkubwa kwa afya na uchumi wa wananchi.

Anthony Onyedikachi, mkurugenzi wa shamba la kufuga konokono la Dikafarms lililoko nje kidogo ya Jiji la Abuja, anasema serikali inaona ufugaji huo kuwa ni “upuuzi,” licha ya kuongeza kipato kwa familia nyingi na kuimarisha afya kwa watumiaji.

“Ufugaji wa konokono haupewi kipaumbele, lakini serikali inakimbilia kodi tu kila tunapouza mazao ya konokono, lakini tukiomba msaada, wanatupuuza, ni hatari sana kuwa na ubaguzi wa wazi,” anasema Anthony.

Konokono wengi wa Nigeria, hasa aina ya African Giant, huuzwa China na nchi za Sweden na Norway, wanaelezwa kuwa na vitamini nyingi na kuwa na virutubishivya kuimarisha kinga ya mwili kwa watumiaji.

Tanzania hali ikoje? Ufugaji wa konokono haujashamiri, lakini wapo wafugaji wadogo wasiojulikana na soko lao haliko wazi sana, ingawa inasemekana wapo Wachina jijini Dar es Salaam hununua kwa kaisi kidogo cha fedha.

### Uganda

## Rughani kung'ara

### Uganda

**M**TALAM wa fedha na uchumi ambaye aliipaisha kiutendaji na kukua kwa kasi Benki ya Standard Chartered Tanzania, Sanjay Rughani, sasa anahamisha ujuzi wake nchini Uganda.

Rughani ambaye ni Mtanania, anasifika kwa weledi na namna anavyotumia mwanya wa kuvumbua bidhaa mpya katika sekta ya benki.

Kwa wanaopenda kufuga, Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine kilichopo Morogoro, ndiyo mahali sahihi pa kufuatilia kupata tutaalam huo.



### Rwanda

## Bingwa wa kwanza kupasua kichwa

**R**WANDA hatimaye imepata daktari wake kwa kwanza mwanamke kuwa bingwa wa kufanya upasuaji wa kichwa na uti wa mgongo.

Daktari Claire Karekezi ni mhitimu wa Chuo Kikuu cha Mohamed V, Rabati nchini Morroco na sasa anafanya kazi katika Hospitali ya Jeshi la Rwanda.

Rais Paul Kagame amepongeza kile alichoeleza kuwa ni uzalendo wa Dkt. Claire kwamba angeweza kwenda kufanya kazi Ulaya ama Marekani, lakini ameamua kuendelea na ujuzi wake adhimu kuokoa maisha ya wananchi nchini kwake.

## Uhuru anaondoka aking'ang'ana kukopa

Na Mwandishi Wetu

**I**MEKUWA kawaida kwa viongozi wengi wa nchi za Afrika kupenda utajiri kuliko kuwatumikia wananchi waliowachagua kuingia madarakani.

Tamaa hii imewafanya viongozi hao kuendelea kubakia madarakani kwa muda unaopitiliza matakwa ya katiba za nchi zao kwa visingizio vingi ikiwamo “kupendwa na umma” au “kulazimishwa na wananchi.” Hivi ni visingizio ambavyo – mara nyingi, havina mashiko, isipokuwa tamaa ya madaraka na dhambi ya kujikusanyia mali.

Hata hivyo, hali hii ni tofauti kidogo na Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, ambaye anaonekana kutofuata nyayo za viongozi wengi wanaokuwa madarakani.

Uhuru hajawahi kusikika akitamani kuendelea kushika madaraka, au kudai anapendwa sana na Wakenya. Sababu zipo nyingi kwa kiongozi huyo aliyebakiza wiki tatu kuondoka Ikulu ya Nairobi. Moja ya sababu hiyo ni Kenya kuwa na Katiba isiyolea dhambi hiyo na pili; “ugumu wa kuongoza” – kama ambavyo amekuwa akisema mwenyewe.

Pamoja na dhambi ya tamaa ya madaraka kumuepuka Rais Uhuru, lakini anaonekana kushindwa dhambi ya kuachia warithi wao madeni makubwa ya nchi na pengine kukausha hazina kabla ya wao kuondoka madarakani.

Dhambi hii imemtafuna pia Rais Uhuru, kwani imebainika kuwa, miezi mitatu kabla ya kuondoka Ikulu, amekopa Shilingi za Kenya bilioni 300.

Kiasi hiki cha fedha kimekopwa na Serikali ya Uhuru kati ya Januari na Mei, 2022.

Hatawa hii kwa mizania yoyote, ni kuongeza mzigo wa madeni kwa Wakenya, nchi yenye idadi kubwa ya watu masikini na sasa deni la taifa hilo la Afrika Mashariki limefikia Sh. trilioni 8.5.

Idadi kubwa ya wachumi waliozungumza na Pambazuko wanaeleza kuwa Kenya inaachwa na Rais Uhuru



Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta

ikiwa na mzigo mkubwa wa madeni kuliko kipindi chochote cha watangulizi wake na kwamba wakati wa uongozi wake wa miaka 10, Kenya imeshuhudia kupromoka kwa thamani ya shilingi yake dhidi ya dola ya Marekani. Hivi sasa dola moja ni sawa na Sh. 118.25.

Takwimu kutoka Hazina ya Kenya zinaonyesha Kenya imekuwa kinara wa kukopa fedha kutoka taasisi za fedha za ndani na nje liendelea kukopa kutoka kwa mashirika ya kifedha ya humu nchini na yale ya kigeni ndani ya kipindi hicho hadi kiwango cha asilimia 69.1 cha utajiri wa nchini kutoka asilimia 66.7 mnamo Januari.

Thamani ya Shilingi ya Kenya ilidorora kwa kiwango cha asilimia 0.8 katika kipindi hicho, kutoka Sh115 kwa dola moja mnamo Januari hadi Sh118.25 kwa Julai na inatarajiwa kuendelea kudorora.

Kwa utaratibu huu wa Rais Uhuru kuendelea kukopa, maana yake ni kuachia mrithi wake madeni makubwa na kuna hisia ataacha Hazina ikiwa “nyeupe.”

Zimebaki siku 22 Wakenya kuamua



### Assange awekwa selo bila nguo



*Picha mbalimbali za Assange tangu alipokuwa kijana, alipokimbia Marekani na anvayoonkana sasa akiwa gerezani.*

#### Na Tryruckia Mfinanga

**J**ULIAN Assange, mwanzilishi na mhariri wa mtandao wa WikiLeaks anayetakiwa kwa udi na uvumba nchini Marekani ili akateswe, kufungwa au hata kunyongwa, ameswekwa selo bila nguo kwa kuhofia kujinyonga.

Hivi sasa Assange anashikiliwa ndani ya gereza la Belmarsh jijini London, Uingereza ambako “ametupwa” chumba cha selo akiwa mtupu baada ya kuhofia kwamba anaweza kutumia nguo kujinyonga kutokana na Serikali ya Uingereza kupitisha uamuzi wa kumpeleka kwa nguvu Marekani kukabiliana na kesi yake.

Waziri wa Mambo ya Ndani wa Uingereza, Priti Patel alitia saini hati ya Assange kupeleka Marekani kukabiliana na kesi yake.

Assange alikimbilia nchini Uingereza mwaka 2012 na kuomba hifadhi katika Ubalozzi wa Equador, baada ya Marekani kutangaza kumkamata na kumfungulia mashtaka ya uhaini na kuhatarisha usalama wa taifa hilo kubwa duniani. Hata hivyo, baadaye ubalozzi huo ulimundoa kwa shinikizo la Uingereza na

kumuweka rumande hadi sasa.

Mhariri huyo alidukua taarifa za siri za Marekani na mataifa mengine na kuanika kwenye mtandao wake kile kinachoelezwa kuwa ni hujuma dhidi ya ustawi wa nchi hiyo. Ikiwa atapatikana na makosa, anaweza kufungwa hadi miaka 175.

Hivi karibuni, baba wa Julian, aitwaye Shipton aliwaambia waandishi wa habari katika Jiji la Berlin, Ujerumani kwamba mtoto wake amedhalilishwa sana na uongozi wa gereza hilo na kumshutumu wserikali yanUingereza kwa kumuonea kijana wake.

“Wafanyikazi wa gereza baada ya kupata taarifa za kupeleka Marekani, walimuona amejawa wasiwasi na msongo wa mawazo, na kuhisi kwamba anaweza kujiua, hivyo kuamua kumvua nguo zote, hii haifai,” aliongeza baba Assange.

Familia ya Assange imesema kwamba inajipanga kwenda mahakamani kupinga uamuzi huo wa serikali ya Uingereza kumpeleka kwa nguvu ili kukabili mashtaka.

Je, Assange ni mhalifu wa uhuru wa kujieleza, sifa inayotamba nayo Uingereza na Marekani kwamba ni moja ya nguzo za ustawi wao? Tafakari.





Na Evarist Chahali  
evarist@chahali.com

## Mezani kwa Chahali

# Nasubiri muujiza kuheshimu Katiba Mpya

Na Evarist Chahali

**W**AKATI mjadala wa Katiba mpya, ambao mara nyingi huambatana na ajenda ya Tume Huru ya Uchaguzi, wahusika wakuu wameendelea kuwa wanasiasa na vyama vya siasa.

Kwa muda mrefu mjadala huo umekuwa ajenda muhimu – na pengine kuu – ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema. Baadaye, chama cha ACT-Wazalendo nacho kikaanza kuongelea kwa sauti kubwa kuhusu suala hilo, japo mtazamo wa chama hicho ni “Tume Huru kwanza kuelekea kupata Katiba Mpya.”

Na karibuni, chama tawala – Chama Cha Mapinduzi (CCM), nacho kimejiingiza kwenye mjadala wa haja ya kupata Katiba

Mpya, ingawa yafahamika bayana kwa muda mrefu, chama hicho kimekuwa kikwazo dhidi ya kupatikana Katiba mpya. Katika toleo lililopita, niliandika kwa kuhoji kama CCM inaweza kuaminika katika suala hilo.

Lakini, lengo la makala haya siyo kuongelea tena Katiba Mpya, bali kuamsha tafakuri kwa kutupia jicho majanga matatu yanayotajwa kuitesa Tanzania kwa sasa: ushoga, usagaji na ulawiti.

Taarifa mbalimbali zinaeleza kuwa vitendo hivyo siyo tu vimetapakaa, bali pia vinazidi kuongezeka kila uchao, huku vijana wengi wakijiingia katika uhusiano wa hovyo wa aina hizo – na pengine bila woga.

Isiyokuwa bahati, au pengine kwa makusudi – vyombo vya habari vimekuwa kimya, havihusiki sana kuandika kwa

kukemea tabia hiyo inayoonekana kumea zaidi mijini.

Lakini hilo siyo gumu kulielewa kwani jamii nayo imekaa kimya kuhusu majanga hayo, kana kwamba hakuna kinachoendelea na pengine hakiihusu..

Kwa mujibu wa uchunguzi usio rasmi niliofanya siku za nyuma, vitendo vya ushoga na usagaji vinachangiwa zaidi na upungufu wa kimaadili katika ngazi ya familia. Kimsingi, vitendo

hivyo vinaotoa mwanya kwa janga la ulawiti dhidi ya watoto wadogo kugeuka janga zaidi.

Tofauti na vitendo vya ushoga na usagaji, vitendo vya ulawiti dhidi ya watoto wadogo vinahusishwa zaidi na imani za kishirikina, ingawa pia wapo wanaojihusisha kwa tamaa zao za hovyo.

Unaweza kujiuliza, “ushoga, usagaji na ulawiti na Katiba Mpya wapi na wapi? “Jibu langu ni kwamba, hata kama Tanzania itafanikiwa kupata hiyo Katiba kila baada ya saa 24 hakutokuwa na matokeo kusudiwa, endapo jamii itaendelea kupuuzia majanga yanayoikabili, ikiwa ni pamoja na hayo ya ushoga, usagaji na ulawiti.

Mimi ni miongoni mwa watu wachache wanaoamini kuwa licha ya ukweli kwamba kuna haja ya kupata Katiba Mpya – au pengine kuifanyia marekebisho Katiba iliyopo – tatizo kubwa lipo miongoni mwa Watanzania wenyewe. Tuna upungufu mkubwa kimaadili, na hiyo inasababisha kutoheshimu sheria. Na kwa vile Katiba ni “sheria mama”, siyo ajabu kushuhudia katiba iliyopo ikipuuzwa.

Je, kama Katiba iliyopo inapuuzwa, miujiza gani itakayowezesha Katiba mpya kuheshimiwa?

## Tishio la wafamasia feki

### Na Waandishi Wetu

**B**ILA shaka, mtu yeyote anayepatikana kodi jeupe ataonekana kuwa daktari au mfamasia aliyehitimu, lakini mtu huyo anayesimama mbele ya makasha na chupa za dawa anaweza kuwa muuaji wako, badala ya kuwa mwokozi anayetarajiwa.

Hali hii ya kuwepo wafamasia wengi wanaouza dawa, inaweza kuonekana neema kwa nchi kwa kuwa na idadi kubwa ya wataalamu hao.

Lakini uchunguzi uliofanywa na Pambazuko, unaonyesha kuwa watu wengi wanaouza dawa na pengine kutoa ushauri wa kitabibu, siyo wataalamu waliosomea taaluma hiyo muhimu.

Pambazuko imebaini kuwa kuna idadi kubwa ya wauza dawa za binadamu wasiokuwa na taaluma hiyo, huku wengine wakiwapa wagonjwa ushauri wa kitabibu kuhusu magonjwa yao.

Pamoja na kutokuwepo takwimu sahihi za idadi ya wauza dawa wasiokuwa na taaluma hiyo, lakini Pambazuko limebaini vijiji vya mikoa wa Tanga na Manyara, vinaweza kuongoza kwani hata maduka ya dawa mengi hayajasajiliwa.

Kutokana na hali hiyo, hivi karibuni, Serikali ya Tanzania, kupitia Baraza la Famasia Tanzania (PC) ilianzisha msako wa nchi nzima dhidi ya maduka ya dawa ambayo hayajasajiliwa na pia kuwa na wakemia wasio na sifa. Jumla ya maduka 23 ya biashara yalifungwa katika Jiji la Dar es Salaam, kitovu cha biashara nchini humo.

Katibu na msajili wa baraza hilo, Elizabeth Shekalaghe aliliambia Pambazuko kuwa msako mkali wa kuwafichua na kuwachukulia hatua za kisheria wamiliki wa maduka ya dawa ambayo hayajasajiliwa ni endelevu na utafanyika nchi nzima.

Takwimu zinaonyesha kuwa Tanzania,

Kenya na Uganda, zinaweza kuwa na maduka ya dawa 7,000 ambapo asilimia 81% yapo vijijini, hivyo wanaojifanya wafamasia, wasiokuwa na sifa - wanaofanya kazi za kitaaluma kinyume cha sheria, wanaweza kuwa wengi zaidi hivyo kuhatarisha maisha ya watu.

Tanzania inatajwa kuwa na wafamasia 3,040 waliosomea taaluma, kusajiliwa na kuthibitishwa na serikali. Kwa kukokotoa, kila mfamasia mmoja anahudumia watu 19,737.

Mbali na changamoto ya kuwa na wafamasia feki, uchunguzi zaidi uliofanywa kwenye viunga vya Dar es Salaam umebaini kwamba maduka mengi ya dawa yasiyokuwa na wataalamu, yamekuwa yakiuza na kutoa maelekezo ya matumizi kwa dawa zinazohitaji utaalamu na uchunguzi mkubwa wa mgonjwa kabla ya kutolewa.

Miongoni mwa dawa inayouzwa zaidi – kwa kutolewa kiholela ni Ceftriaxone - ambayo inajulikana kwa jina la biashara; Powercef.

Uchunguzi wa Pambazuko uliofanywa kwa wiki tatu katika vituo vitatu vya afya na kliniki za kibingwa wilayani Kinondoni, umethibitisha kuwa wagonjwa wengi wanaofika kupata matibabu, asilimia 90 wamekuwa wakitibiwa kwa Powercef, dawa inayoelezwa kutibu magonjwa mengi.

Wagonjwa wengi waliotibiwa kwa dawa hiyo, iliyobatizwa jina la “Sindano ya Mungu” na baadhi ya madaktari, waliozungumza na Pambazuko, wamesema hutibu kwa haraka zaidi magonjwa ya kifua, udhaifu wa mwili na maambukizi katika damu.

Madaktari waliohojiwa walisema Powercef ni miongoni mwa dawa zinazochomwa kwenye mishipa, zenye uwezo mkubwa wa kupambana na magonjwa anuai, ambapo pia hutibu kwa haraka

---

## **Tishio la wafamasia feki**

homa ya uti wa mgongo, nimonia, maambukizi kwenye njia ya mkojo, magonjwa ya zinaa na maambukizo mengine ya bakteria.

Katika vituo ambavyo waandishi wetu walitembelea, sindano moja ya Powercef inauzwa kwa Sh. 7,000 (Dola za Marekani 2.70).

Dkt. Isaac Maro, mmoja wa matabibu mashuhuri nchini, amekiri matumizi makubwa ya dawa hiyo akitaja sababu mbili za madaktari “kukimbilia” Powercef; uvivu wa baadhi ya madaktari katika kuchunguza sababu halisi za ugonjwa na kujipatia fedha za haraka.

“Kuna ushahidi wa wazi kwamba Powercef inatumika kupita kiasi, na mbaya zaidi hata baadhi ya maduka ya dawa au zahanati, wanaojita madaktari wanaiuzwa kiholela...”

... Dawa hii ya vijiuasumu (antibiotic) ina nguvu, ni madaktari waliohitimu vyaoni tu ndio wanaoruhusiwa kuwapatia wagonjwa baada ya matokeo ya uchunguzi wa maabara ya kitabibu, siyo vinginevyo,” anaonya.

Dkt. Isaac anaeleza kuwa miongoni mwa madhara makubwa kwa matumizi holela ya dawa, hasa vijiuasumu ni kujenga usugu kwa magonjwa, kuongezeka kwa magonjwa ya ini na pia kupunguza nguvu ya kinga kwa watu.

Naye Mganga Mfawidhi wa zahanati ya Nyota Njema iliyopo Mwenge, Dar es Salaam, Kassim Mwaluko, anasema Powercef ambayo haipendekezwi kutumika kwa watoto wachanga na wanaozaliwa kabla ya wakati kutokana na hofu ya kuongezeka kwa hatari ya madhara, inapaswa kutumiwa kwa uangalifu mkubwa na wahudumu wa afya waliopewa mafunzo.

“Powercef, kama jina linavyoonyesha, ina nguvu na ufanisi katika kutibu baadhi

ya maambukizi, lakini inaweza kuleta madhara ikiwa inatumiwa vibaya na mara kwa mara kwa magonjwa; kwa hivyo, haiipaswi kuchukuliwa kama tiba ya kwanza kwa kila ugonjwa,” anaonya.

Dk. Mwaluko anawasihi madaktari wenzake kumtibu mgonjwa kwa Powercef tu baada ya uchunguzi wa kimaabara ili kuepuka kuwa sugu kwa matibabu.

Naibu Waziri wa Afya, Dkt Godwin Mollel akizungumza na Pambazuko anasema kuwa madaktari wanapaswa kuwa makini na dawa ambazo zinahitaji matokeo ya uchunguzi wa kimaabara kabla ya kutumika kwa mgonjwa.

“Mara nyingi serikali imekuwa ikiagiza matumizi makini ya dawa – hasa za vijiuasumu na zisitumike kiholela, hasa zile zenye kuhitaji matokeo ya maabara,” anaozungeza Dkt Mollel.

Mganga Mkuu wa Serikali Tanzania, Dkt. Aifello Sichelwe anakiri dawa hiyo imeonekana kutumika zaidi katika kipindi cha miaka miwili iliyopita kutokana na kuwepo matatizo mengi ya mfumo wa upumuaji.

Dkt. Sichwale anasema pia mahitaji makubwa yanaweza kuwa ni matokeo ya ufanisi wa dawa hiyo pamoja na upatikanaji wake nchini, lakini pia anawashauri madaktari kutoitumia kiholela kama tiba ya kwanza kwa kila mgonjwa.

“Nina matumaini sana kwamba madaktari wanajua wakati na jinsi ya kuagiza mgonjwa atibiwe kwa Powercef, lakini lazima wawe waangalifu wasiitumie vibaya ili isiwe sugu kwa sababu ya kutumiwa kupita kiasi,” anaonya.

Hivi karibuni, Shirika la Afya Duniani (WHO) lilitangaza kuibuka kwa kasi kwa matumizi ya dawa za vijiuasumu katika nchi za kitropiki kutokana na kuwepo kwa maambukizi ya Corona na kuonya matumizi holela ya dawa hizo.

### Bill Gates kujiondoa kwenye utajiri



**Bilionea Bill Gates wa Marekani**

**P**AMOJA na 'raha' ya kuwa na fedha nyingi zaidi, bilionea Bill Gates wa Marekani ameahidi kutoa sehemu kubwa ya mali yake kusaidia watu masikini, ili aodoke kwenye orodha ya matajiri zaidi duniani.

Tajiri huyo wa nne duniani amesema ana wajibu wa kuchangia kupunguza madhila ya nchi masikini hasa katika nyanja za elimu, afya na maji ili kuokoa maisha, lakini pia kuleta ustawi wa watu wake.

Mwanzilishi huyo mwenza wa Kampuni ya Microsoft, amekuwa akitoa misaada ya fedha na utaalamu kupitia wakfu aliyozanzisha na mkewe wa zamani, Melinda (Bill and Melinda Gates Foundation).

Gates ameahidi kuchagua zaidi dola za Marekani bilioni 20 mwezi huu, hivyo kupunguza kwa kiasi kikubwa sehemu

ya utajiri wake unaotajwa kufikia bilioni 118, kwa mujibu wa jarida la Forbes.

Katika mtandao wa Twitter, Gates amesema wakfu huo utaongeza matumizi yake kutoka dola za Marekani bilioni 6 kwa mwaka hadi bilioni 9 ifikapo 2026 ili kukabili majanga na changamoto za mataifa masikini zaidi duniani.

“Ninajipanga kwa siku chache zijazo kutoa karibu mali yangu yote kwa wakfu,” alisema na kuongeza; “nitashuka na hatimaye kutoka kwenye orodha ya watu matajiri zaidi duniani...”

“Nina wajibu wa kurudisha sehemu ya rasilimali zangu kwa jamii ili kupunguza shida na mateso makubwa kwa watu, ni wajibu wangu kufanya hivyo kama ambavyo nimekuwa nikifanya.”

Wakfu wa tajiri huyo inafanya kazi katika nchi nyingi hasa kwa kutokomeza magonjwa kama malaria, kuboresha elimu na kukabiliana na kupatikana kwa maji.

Inakadiriwa kuwa wakfu huo ndiyo unatajwa kutoa fedha nyingi zaidi kwa watu masikini na kuwa matajiri wengine, akiwamo Warren Buffet huongeza kiasi kikubwa cha fedha ili kufanya kazi zake.

Wakfu huo ndio mfidhili mkubwa zaidi wa misaada kwa Shirika la Afya Duniani (WHO) na taasisi zingine za misaada kwa nchi masikini zaidi.

Bill Gates alishikilia taji la Forbes la kuwa mtu tajiri zaidi duniani kati ya 1995 na 2010 na tena kutoka 2013 hadi 2017.

Hivi sasa mwanzilishi wa Kampuni ya Amazon ya Marekani, Jeff Bezos ndiyo alimuondoa gates kwenye nafasi ya tajiri zaidi duniani mwaka 2017. Hata hivyo, miaka miwili iliyopita, naye ameondolewa kwenye nafasi hiyo na sasa inashikiliwa na mmiliki wa Kampuni ya Tesla, Elon Musk.

• **Sehemu kubwa ya makala haya imetoka BBC**

# Atamani Zanzibar yenye neema



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Othman Masoud Othman (Picha:BBC)

## Na Jabir Idrissa, Unguja

**S**ERIKALI ya Umoja wa Kitaifa (SUK) anayoitamani mtaalamu mboenzi wa sheria, Othman Masoud Othman ni ile inayoelekeza kujengea nchi mazingira bora ya siasa, uongozi shirikishi na maendeleo endelevu kwa watu wa Zanzibar.

Anatamani kuona matunda ya nchi yanawafikia wananchi wote bila ubaguzi wa rangi, maeneo wanakotoa ama kuishi na bila kujali ushabiki ama ufuasi wa vya-ama vya siasa.

Othman ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, anaeleza kuwa kinyume cha misingi hiyo na kushindwa kutekelezwa kwa ahadi za kuimarisha SUK, ni serikali kujichimbia kaburi ambalo linaweza kufukia hata wale wanaohusika kukandamiza na kuminya ustawi wa jamii ya watu wa Zanzibar.

Anaeleza kwamba kukua kwa mgawanyiko katika jamii kunachagiza chuki miongoni mwa wananchi na kusababisha machungu makubwa ikiwamo uonevu wa dhahiri kwa wenye mawazo kinzani na watawala wenye dola.

Moja ya misingi ya kuhakikisha Zanzibar inakuwa na amani muda wote, ni kuwepo kwa Tume Huru ya Uchaguzi ambayo itakuwa msimamizi wa haki wa mchakato mzima wa kufanyika kwa uchaguzi huru, haki na wenye kuleta viongozi walioshinda kihalali kupitia sanduku la

kura.

Mwanasheia Othman aliyewahi kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali Zanzibar, anaeleza kuwa tume iliyopo imekuwa kiini cha matatizo yanayokwamisha maendeleo kiuchumi na kuminya matakwa ya wananchi katika uongozi wa nchi yao.

Othman alieleza hayo hivi karibuni alipokutana na Balozi Mdogo wa Uingereza nchini Tanzania, Rick Shearn aliyemtembelea ofisini kwake Migombani, mjini Zanzibar kwa mazungumzo maalum.

Balozi Shearn alieleza matumaini ya nchi yake kusaidia Zanzibar kutekeleza sera za kupambana dawa za kulevya, kuendeleza hifadhi ya mazingira na kukabili athari za mabadiliko ya tabianchi, maridhiano, umoja wa kitaifa na ujenzi wa mifumo bora ya kuchochea mageuzi ya kisiasa.

Maoni ya Othman yanakuja kipindi ambacho fikra za watu wengi zinahimiza kuwepo utashi wa kisiasa, hasa kutoka chama tawala, Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika kushirikiana na vyama vingine, kuchochea mshikamo wa Wanzibari na kuhimiza maendeleo ya pamoja.

Kuna kila dalili kwamba CCM inapendelea zaidi kuona serikali inayoundwa na chama hicho pekee, bila kujali dhamana ya kura – kwa asilimia kubwa kutoka chama kingine na kupuuza misingi ya SUK.

---


### Tutakumbuka Daima...



*KWAMBA Kenneth Kaunda ndiye muasisi na rais wa kwanza wa Zambia, nchi iliyopata uhuru kutoka kwa koloni la Uingereza Oktoba 24, 1964. Kabla ya uhuru huo, nchi hiyo ilikuwa ikijulikana kwa jina la Northern Rhodesia. Zambia ni jina lililotokana na Mto Zambezi. Kaunda sasa ni marehemu – alifariki Juni 17, 2021 baada ya kuugua nyumonia akiwa na umri wa miaka 97. (Picha kutoka Maktaba ya Pambazuko).*

---

## Jifunze salamu za Kiswahili



Na Dkt. Michael Mashauri

**K**ISWAHILI ni miongoni mwa lugha zinazokua kwa kasi kubwa kila siku duniani. Vyuo vikuu nje ya Afrika, vimeanza kufunza lugha hiyo adhimu. Kutokana na umuhimu wake, Pambazuko limeamua – kila wiki, kuwa njia ya kufundisha Kiswahili bure kwa yeyote anayependa.

Leo Mwalimu anazungumzia juu ya salamu (greetings) za awali za lugha hiyo.

Kuna salamu rasmi na zisizo rasmi katika Kiswahili (Kiswahili has formal and informal greetings).

### Salamu rasmi (Formal greetings)

Hutumika katika miktadha rasmi na isiyo rasmi (Used in formal and informal contexts).

### Mifano (Examples)

Zawadi: Habari (gani) Furaha? (How are you Furaha?)

Furaha: Nzuri, (Fine)

Zawadi: Hujambo? (How are you doing?)

Furaha: Sijambo Zawadi, wewe je? (I am fine, how about you?)

Zawadi: Mimi pia (sijambo) (Me too (I'm fine))

Neno 'gani' linaweza kubadilishwa na: yako/zenu (umoja/wingi), za saa hizi, za nyumbani, asubuhi, jioni, mchana, usiku au huko na jibu linabaki kuwa 'nzuri' (The word 'gani' can be replaced by yako/zenu (your), za saa hizi (of this time), za nyumbani (of home), za asubuhi (morning), za jioni (evening), za mchana

(noon), za usiku (night), za huko (their) and the response is still 'nzuri'.

Unaweza pia kutumia maneno haya bila neno 'habari' na jibu lake bado ni 'nzuri' (You can also use these words without 'habari' and the reply is still 'fine'). Mfano:

(Habari) za asubuhi (Good morning)

(Habari) za mchana (Good afternoon)

(Habari) za jioni/usiku (Good evening)

(Habari) za kazi/safari/masomo (H o w

was the work/journey/studies?)

(Habari) za nyumbani (How is home?)

Jibu: Nzuri (Response: Fine)

'Shikamoo' hutumika kwa mdogo kumsalimu mkubwa kiumri ('Shikamoo' is used by younger people to elders).

Sifa: Shikamoo baba (Shikamoo daddy)

Baba: Marahaba Sifa, hujambo?

(Marahaba Sifa, how are you?)

Sifa: Sijambo baba (I'm fine daddy)

Baba: Umeamkaje/Umelalaje/

Umeshindaje (How have you woken up/slept/how was your day?)

Sifa: Salama (Fine)

Utamaduni: Katika Kiswahili watu husalimiana kabla ya kuanza kufanya kitu chochote. Wale wenye heshima na wakubwa huanza kusalimiwa. Salamu huweza kuambatana na kushikana mikono. (Cultural notes: Usually in Swahili people greet each other before engaging in anything. Those considered to have high status or elders are greeted first. Greetings may be accompanied by shaking hands).

• **Mwandishi wa Darasa la Kiswahili ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.**



### Eacop: Tunajali haki za jamii za pembezoni

**Na Mwandishi Wetu, Manyara**

**M**RADI mkubwa wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi wa Afrika Mashariki (Eacop) unatekeleza shughuli zake kwa kuzingatia haki za binadamu kwa watu wote wanaoguswa na mchakato wa kukamilisha mradi huo.

Pamoja na kuzingatia haki za binadamu, Eacop inajali haki na maisha ya jamii za pembezoni ambazo zinatajwa kuwa na mahitaji maalum.

Meneja Mkuu wa Eacop kwa upande wa Tanzania, Wendy Brown, Julai 6, mwaka huu akiwa Kitongoji cha Napilikunya, Man-yara alisema kampuni hiyo ya bomba la mafuta inafuata taratibu zote kuhakikisha kwamba watu wanaoguswa na mradi huo, hawapotezi hadhi ya maisha yao wakati wa kutekelezwa kwa shughuli kutandaza bomba hilo la mafuta unaohusisha nchi mbili za Afrika Mashariki; Tanzania na Uganda.

Wendy alisema kampuni yake imejizatiti kufuata sheria zote za Serikali ya Tanzania na taratibu za kimataifa, hasa Benki ya Dunia katika kutekeleza shughuli zake bila kuathiri maisha ya watu wanaoguswa na mradi huo mkubwa na wa kimkakati.

Eacop imekuwa katika mazungumzo ya muda mrefu na jamii ya watu wa kabila la Akie wanaoguswa na mradi huo wa bomba ili kupata muafaka wa namna

ya kuzingatia maisha, mila na desturi zao kabla ya kuanza utekelezaji.

Wiki iliyopita, Eacop na uongozi wa serikali na jamii ya Akie waliingia mkataba wa mpango kazi na makubaliano ya ridhaa huru ambapo jamii hiyo itapata fursa zinazotokana na kuguswa na mchakato wa kutandaza bomba hilo linalopita kwenye baadhi ya maeneo yao.

Mshauri wa Eacop kuhusu jamii za pembezoni, Dkt. Elifuraha Laltaika alis-ema kwa furaha, "Ninajivu-nia ukweli kwamba Tanza-nia imekuwa miongoni mwa nchi chache katika ukanda wa Afrika kutekeleza rid-haa huru ya mpango mpya na kabambe wa sheria za kimataifa unaohitaji ush-irikishwaji wenye tija kwa jamii za pembezoni kabla ya kutekeleza mradi katika ardhni ya Akie.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya ya Kiteto, Fad-hili aliipongeza Eacop kwa ushirikiswaji wenye tija ambao umefanya shughuli za mradi wa bomba kufanyika bila kizuizi katika wilaya hiyo kwa kuwa imefuata vigezo vya kimataifa.

Ridhaa Huru ya Uelewa Kabla ya Utekelezaji wa Mra-di (FPIC) ni kigezo muhimu kilichowekwa na mashirika ya fedha ya kimataifa na sheria za haki za bin-adamu ili kuzingatiwa wakarti wa utekelezaji wa miradi mikubwa ili kulinda ardhni na urithi wa asili wa jamii za pembezoni.



Mshauri wa Eacop kuhusu jamii za pembezoni, Dkt. Elifuraha Laltaika (kushoto), akifuatiwa na Meneja Mkuu wa Eacop - Tanzania, Wendy Brown, kiongozi wa mila wa Jamii ya watu wa Akie, Oringidi Masuny, mwenyekiti wa kitongoji, Pasinai Oltingi, mwenyekiti wa jami ya Akie wa Napilikunya, Yohana Lemana na kiongozi wa kitaifa wa jamii ya Akie, Elias Rumas, wakionyesha mkataba wa makubaliano kwa furaha. (Picha: Hisani ya Eacop).

## Mpemba: Mtanzania kijana aliyetikisa dunia ya utafiti - 2

Na Mwandishi Maalum

**KATIKA toleo lililopita, Mtanzania – mwanafunzi wa sekondari, aliyetikisa dunia ya watafiki, Erasto Bartholomeo Mpemba, kwa kugundua kuwa maji ya moto huganda haraka zaidi kuwa barafu kuliko maji yenye ubaridi. Sasa endelea na makala haya...**



**S**wali lake kwa mara nyingine likaibua mabishano kati ya Mpemba kwa upande mmoja, mwalimu na wanafunzi wenzakewa upande wa pili. Mwalimu akaendelea kusisitiza kuwa kimiminika chenye joto kali, hakiwezi kuganda haraka kuliko chenye ubaridi.

Mwalimu alieleza kuwa hilo haliwezekani kisayansi, huku Mpemba naye akijenga hoja kuwa japo hakuna maelezo ya kutosha kisayansi, lakini yeye amelishuhudia hilo likitokea kwa macho. Mwalimu na wanafunzi wenzake hawakumuamini kabisa.

Pamoja na ushuhuda wake kukataliwa

na wanafunzi pamoja na mwalimu, bado Mpemba alisimamia alichokiona, aliamini siyo kila matokeo yalipaswa kwenda sambamba na hali iliyozoeleka na alitaka wenzake wakubali matokeo mapya tofauti na yale waliyoyazoea. Mwalimu baada ya kuchoshwa na udadisi wa Mpemba, aliamua kuufunga mjadala huo wa kitaaluma kwa kebehi kuwa “huo utafiki na ugunduzi wa maziwa ya moto kuganda mapema zaidi ya maziwa ya baridi kwenye jokofu, utakuwa ni kile alichokieleza kuwa ni “fizikia ya Mpemba” na siyo fizikia ya ulimwengu”.

Baada ya hapo ikawa ndio utani tena, kila alichokikosea shuleni pale kiliitwa ‘Cha Mpemba’, kwa mfano kwenye hesabu za “Alogarithms” alipokosea basi, mwalimu wa somo hilo na hata wanafunzi wenzake walikebehi ni ‘hesabu za Mpemba’ na siyo hesabu za Algorithms! Lakini Mpemba, hakukatishwa tamaa na hali hiyo.

Siku moja akiwa katika maabara ya baiolojia shuleni hapo, aliamua kurudia jaribio lake, lakini badala ya kutumia maziwa mara hii alitumia maji, alijaza kiasi cha maji ujazo sawa kwenye ‘bikari’ (kifaa kidogo kama bilauri ndogo maalum zinazotumika maabara) mbili, moja akaweka maji ya baridi na nyingine akaweka maji ya moto, kisha akaziweka kwenye jokofu kwa muda wa saa moja.

Alipokuja kuziangalia baada ya muda huo, alikuta bikari iliyokuwa na maji ya moto tayari imeanza kuweka barafu nyingi, wakati ile iliyokuwa na maji ya baridi, ikiwa barafu kidogo! Hii ilizidi kumpa uhakika wa ugunduzi wake, ugunduzi uliokataliwa na waalimu wake wawili wa somo la Fizikia pamoja na wanafunzi.

Wakati mmoja wanafunzi wa kidato cha tano na sita Shule ya Sekondari Mkwawa, walipata nafasi ya kutembelewa na Mhadhiri Mwandamimizi wa Chuo

### Mtanzania aliyetikisa dunia

Inatoka Uk. 17



Kikuu cha Dar es Salaam, Dkt. Dennis Osborne (wakati huo akiwa bado ni daktari wa falsafa tu, sasa ni Profesa Osborne) ambaye alikuwa mtaalamu wa Fizikia. Osborne alialikwa shuleni na mkuu wa shule hiyo ili kuhamasisha wanafunzi kusoma kwa bidii ili wafaulu na wafanikiwe kujiunga na masomo ya chuo kikuu.

Huyu alikuwa mtaalamu wa Fizikia, alipata wasaa wa kuzungumza na wanafunzi kuhusu somo hilo, mwishoni wanafunzi walipewa nafasi ya kumuuliza maswali Dk. Osborne. Maswali yalikuwa mengi, yapo yaliyohusu namna ya kujiunga na chuo kikuu, idadi ya wanaotakiwa kuingia chuo kikuu, ugumu na wa somo la Fizikia chuo kikuu, unakuwa nani ukimaliza shahada ya Fizikia na mengine mengi.

Lakini, swali 'lilowavunja mbavu' wanafunzi wengi kama siyo wote, ni swali alilouliza Erasto Mpemba.

Mpemba alimuuliza Dk. Osborne swali lilelile alilowahi kuwauliza mwanzoni walimu wake wawili wa Fizikia, tofauti ikiwa mara hii akiuliza kuhusu maji na siyo maziwa, na akiwa makini zaidi kujua joto-ridi la awali la maji yake, alimuuliza "inakujaje ukijaza maji ya moto yenye

nyuzi joto 100 za sentigredi na maji baridi yenye nyuzi joto 35 za sentigredi, kwa ujazo sawa kwenye bikari mbili tofauti kisha ukaweka kwenye jokofu, maji yaliyokuwa na nyuzi joto 100 yanaganda kabla ya yale yaliyokuwa na nyuzi joto 35?"

Dk. Osborne, kwanza alicheka kama walivyocheka wengine katika hadhara ile, kisha akamwambia Mpemba arudie swali lake. Mpemba akarudia kilekile alichokiuliza mara ya kwanza, mara hii Dkt. Osborne alisikiliza kwa makini zaidi, mara baada ya Mpemba kurudia swali lake akamuuliza - "una hakika umefanya hivyo?"

Mpemba akajibu ndio, nina hakika nimefanya, ndipo Osborne alitaka kujiridhisha kama kweli alichosikia ndicho kilichoulizwa, pili alitaka kujua imani ya muuliza swali juu ya anachokiuliza na tatu na alitaka kujua chanzo cha hoja, ndo maana akamuuliza endapo Mpemba alifanya uchunguzi mwenyewe. Baada ya kujiridhisha na yote hayo alijibu swali la Mpemba kwa kumwambia kuwa "sijui kwa kweli, lakini nakuahidi kuwa nitajaribu huo uchunguzi nikifika Dar es Salaam".

**Itaendeela wiki ijayo...**

---

---

Jumatatu, Julai 18, 2022

**Pambazuko**

19

*Michezo*

---

**Ubingwa Yanga ni mikakati**

---

## PICHA KUBWA

*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, akizungunza na Sasha Mbilinyi, binti wa aliyewahi kuwa Mbunge wa Mbeya Mjini (Chadema), Joseph Mbilinyi 'Sugu.' Hii ilikuwa ni kwenye tamasha la Dream Concert lilitoandaliwa na Sugu Mei 31, 2022 kwa lengo la kutathmini safari ya muziki ya mwaniasia huyo. Shughuli hiyo ilifanyika jijini Dar es Salaam katika Hoteli ya Serena. (Picha: Ikulu).*



*GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi na Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO).*

